

Nafasi ya Biashara za Kimataifa katika Kukuza Uzungumzaji wa Kiswahili kwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari Nchini Rwanda

Emmanuel Niyirora¹ na Wallace K. Mlaga²

Ikisiri

Tafiti zinaonesha kwamba lugha ya Kiswahili nchini Rwanda haizungumzwi vizuri kama lugha nyingine zinazofundishwa nchini humo. Ingawa lugha hii haizungumzwi kwa ufasaha, hasa katika shule za sekondari, wanafunzi wanaojifunza katika baadhi ya shule za sekondari wanapata fursa ya kuchangamana na wazungumzaji wa Kiswahili. Wazungumzaji hao ni pamoja na wazazi, jamaa na marafiki wanaofanya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka. Jambo hili husaidia sana katika uimarishaji wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Makala hii ililenga kutimiza malengo mahususi mawili. Lengo la kwanza lilikuwa kujadili dhana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka na dhana ya uzungumzaji wa Kiswahili na lengo la pili lilikuwa kubainisha mchango wa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Utamaduni Jamii. Mbinu za uchanganuzi wa matini na mahojiano zilitumiwa kukusanya data. Usampulishaji lengwa ulitumiwa kupata sampuli ya utafiti kutoka kwenye shule zilizoteuliwa. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zina mchango mkubwa katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Isitoshe, utafiti huu umependekeza kuwa walimu wanapaswa kutumia fursa ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka katika uimarishaji wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wao.

1.0 Utangulizi

Kiswahili ni lugha ya Kibantu na ya Kiafrika. Asili yake ni sehemu za mwambao au upwa wa Afrika Mashariki. Watu wa mwambao ndio wenye asili ya Kiswahili (Chiragdin na Mnyampala, 1977). Kiswahili hutumiwa na nchi nyingi duniani na kina idadi kubwa ya watumiaji kutokana na umuhimu wake usio kifani. Ilipodhihirika kuwa Kiswahili ni lugha muhimu, siyo tu kwa mawasiliano bali pia katika maendeleo endelevu ya wananchi, nchi tofauti zilitilia mkazo uimarishaji wa Kiswahili. Kutokana na umuhimu huo, viongozi wa nchi hasa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki waliamua kukifanya Kiswahili kiwe lugha rasmi na

¹ Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Rwanda. Barua pepe: e.niyirora@ur.ac.rw

² Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Rwanda. Barua pepe: w.mlaga@ur.ac.rw

ipanuliwe kimatumizi. Hivi sasa, Kiswahili ni lugha rasmi nchini Tanzania, Kenya, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Rwanda. Vilevile, Kiswahili hutumiwa na mamilioni ya watu nchini Burundi, Sudani, Somalia, Msumbiji na Afrika Kusini. Aidha, takwimu za Shirika la Kimataifa la Sayansi, Elimu na Utamaduni (UNESCO) zinaonesha kuwa Kiswahili kinazungumzwa na watu zaidi ya milioni 200 duniani kote. Mnamo mwaka wa 1986, Shirika la Kimataifa la Sayansi, Elimu na Utamaduni (UNESCO) lilipitisha azimio kwamba Kiswahili kitumike kwenye vikao vyake vyote. Hata katika Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Afrika Mashariki, lugha hii ni rasmi kwa ajili ya mawasiliano. Kwa hiyo, wazungumzaji wanaweza kuitumia kutoa hotuba au kuchangia mijadala mbalimbali (Mwakagele, 2016). Ingawa Kiswahili ni lugha muhimu ambayo inahitajika, hasa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, bado kuna changamoto kwenye ufundishaji na namna kinavyotumiwa katika mawasiliano hususani mazungumzo.

Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa Kiswahili ni lugha muhimu katika maisha ya kila siku (Msofe, 2019; Otieno, Inyani na Shikuku, 2020). Kwa hiyo, serikali ya Rwanda ilifanya jitihada za kuimarisha Kiswahili miongoni mwa Wanyarwanda. Ingawa uongozi wa Rwanda ulifanya mambo mengi ili kuimarisha matumizi ya Kiswahili, bado idadi ya Wanyarwanda wenye uwezo wa kuzungumza Kiswahili ni ndogo ikilinganishwa na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki (Tabaro, 2019). Wazo hili linaonesha kwamba uzungumzaji wa Kiswahili bado uko kwenye kiwango cha chini nchini Rwanda. Mawazo ya Morosini na Singh (1994) kuwa mwingiliano wa watu mipakani huweza kuchangia katika ukuaji wa lugha miongoni wa wananchi wa nchi jirani, yametusukuma kuandika makala hii ili kubainisha nafasi ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka katika kukuza uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda.

Aidha, hakujashuhudiwa andiko lolote lililoshughulikia namna biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinavyoweza kuimarisha uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Ukosefu wa tafiti kama hizi huwanyima wadau wa sekta ya elimu taarifa kuhusu namna ambavyo uzungumzaji wa Kiswahili unaweza kuimarishwa kupitia biashara za kimataifa za kuvuka mpaka. Hivyo basi, utafiti umeshughulikia pengo la kiutafiti lililodokezwa hapo juu. Makala hii ni muhimu kwa walimu na wanafunzi wa madarasa ya Kiswahili pamoja na wadau wengine wa sekta ya elimu. Hii ni kwa kuwa, makala inatoa taarifa muhimu kuhusu namna ya kuimarisha uzungumzaji wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi na Wanyarwanda kwa ujumla kupitia biashara za kimataifa za kuvuka mpaka.

2.0 Methodolojia na Nadharia ya Utafiti

Utafiti ulioibua makala hii ulilenga kutimiza malengo mahususi mawili. Mosi, kujadili dhana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka na dhana ya

uzungumzaji wa Kiswahili na pili ni kubainisha mchango wa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Utafiti ulioibua makala hii ulifanywa kwenye shule za mpakani na zile zilizo mbali na mpaka wa Rwanda. Shule za mpakani zilizochaguliwa ni zile ambazo zinakaribiana na nchi ambamo Kiswahili hutumiwa sio tu kama lugha rasmi bali pia kama lugha mama. Shule hizi ni: Rusumo High School, GS Kigina na GS Nyabitare. Vilevile, shule zilizo mbali na mpaka wa Rwanda zilizoteuliwa kwa makusudi ni zile zinazokaribiana na mahali ambapo panapatikana wafanyabiashara kutoka nchi ambazo huitumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zao za kila siku. Shule hizi zilichaguliwa kwa sababu zina wanafunzi ambao wanaweza kuwa na fursa ya kuwasiliana na wafanyabishara wanaozungumza Kiswahili. Shule hizo ni GS Rwamagana A, GS Duha Complexe School na GS HVP Gatagara.

Ili kutimiza malengo ya makala hii, data za kitaamuli zilikusanywa kwa kutumia mahojiano, ushuhudiaji na uchanganuzi wa matini. Zaidi ya hayo, data msingi na za upili zilikusanywa kutoka kwa walimu sita (6) wa Kiswahili na wakurugenzi wa masomo (*Directors of Studies*) sita (6) walioteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa. Sampuli ya utafiti ilitoteuliwa kwenye shule za sekondari za Wilaya za Kirehe na Rwamagana kwa kuwa wilaya hizi zina wafanyabiashara wengi kutoka kwenye nchi zinazotumia Kiswahili. Shule sita ziliteuliwa kwa kuwa ndizo ambazo zinakaribiana na mahali ambapo panapatikana wafanyabiashara kutoka nchi ambazo huitumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zao za kila siku. Walimu walioteuliwa ni wale ambao wanafundisha Kiswahili katika shule teule. Vilevile, wakurugenzi wa masomo waliteuliwa kutoka kwenye shule husika kwa kuwa tuliona kuwa watatusaidia kupata taarifa zinazozihitajika kukamilisha malengo ya utafiti huu. Mbinu za mahojiano na uchambuzi wa matini zilitumiwa kukusanya data ambazo zilichambuliwa na kuchanganuliwa kwa kutumia madondoo na maelezo.

Aidha, ili kukamilisha malengo mahususi ya makala hii, Nadharia ya Utamaduni Jamii ilitumiwa. Nadharia hii iliasisiwa na Vygotsky (1962) anayeeleza mchango wa mwingiliano wa binadamu na wanajamii wanaomzunguka katika maendeleo ya kiakili. Kwa mujibu wa Zubaidi (2015), wazo kuu la Nadharia ya Utamaduni Jamii ni kwamba binadamu anaendeleza ujuzi, maadili na imani zake kupitia mwingiliano wake na wanajamii au kwa kushiriki katika matukio ya kitamaduni. Nadharia hii inashikilia kwamba binadamu hujifunza kupitia mchakato wa kijamii. Hii ina maana kwamba uvumbuzi na ugunduzi huundwa akilini mwa binadamu kutokana na mwingiliano wake na wale walio karibu naye ambao wana ujuzi zaidi. Mhimili huu ulitusaidia kubainisha mchango wa biashara za kimataifa za kuvuka mipaka katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda.

3.0 Dhana ya Biashara za Kimataifa za Kuvuka Mpaka na Uzungumzaji wa Kiswahili

Biashara za kimataifa za kuvuka mpaka ni biashara zinazofanyika kati ya nchi mbili au zaidi. Aina hizi za biashara zinawahusisha wafanyabiashara kutoka nchi tofauti, wanaotumia lugha tofauti na wanaoingia kwenye nchi fulani ili wapate tijara. Biashara za aina hii zinapofanyika nchini Rwanda zinawahusisha wafanyabiashara wa kimataifa wanaoingia kwenye nchi ya Rwanda. Wafanyabiashara hawa huwa wanatumia lugha tofauti na kuwaathiri baadhi ya Wanyarwanda mpaka wakaanza kuzungumza lugha hizo za kigeni. Hivyo basi, utafiti huu ulilenga kujadili dhana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka na uzungumzaji wa Kiswahili katika shule za mpakani na zilizo mbali na mpaka wa Rwanda. Ili kutimiza lengo hili, tulijiegemeza kwenye mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Utamaduni Jamii kwa sababu ndio unaoendana na malengo ya makala yetu. Mhimili huu unatanabahisha kuwa binadamu anaendeleza ujuzi, maadili na imani zake kupitia mwingiliano wake na wanajamii au kwa kushiriki katika matukio ya kitamaduni. Katika muktadha huu, biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinatoa fursa kubwa kwa wanafunzi wa Kiswahili kuwa na maingiliano na wazungumzaji wa Kiswahili. Hivyo basi, sehemu hii imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni dhana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka na dhana ya uzungumzaji wa Kiswahili.

3.1 Dhana ya Biashara za Kimataifa za Kuvuka Mpaka

Katika utafiti ulioibua makala hii, tulikusanya taarifa tofautitofauti kuhusu dhana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka. Data hizi zilikusanywa ili zisaidie kueleza nafasi ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka katika ukuzaji wa Kiswahili cha mazungumzo kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinaelezwa kama shughuli za kununua na kuuza bidhaa kutoka nchi mbalimbali kwa madhumuni ya kupata faida. Biashara za aina hii husababisha wafanyabiashara kuvuka mpaka wa nchi yao na kusafiri kwenda nchi nyingine kwa ajili ya kuuza au kununua bidhaa (Guevara na Teresa, 2019). Taarifa zilizokusanywa kuhusu dhana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka, zilipatikana kutoka kwa walimu na wakurugenzi wa masomo walioulizwa swali hili: “Ni nini maana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka?” Mtoataarifa wa kwanza kutoka upande wa walimu alisema:

Maana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka ni uchuuzi unaofanyika kutoka nchi moja hadi nchi nyingine au nchi za ng'ambo kwa mfano, Wanyarwanda kufanya biashara na Watanzania, Wakenya, Warundi na wengineo. Biashara hizi huwezesha wafanyabiashara kufika kwenye soko la kimataifa na kuwafanya washindani wa faida katika mataifa mbalimbali.

Chanzo: Data za Uwandani (2023)

Dondoo hili linaonesha kwamba biashara za kimataifa za kuvuka mpaka ni biashara ambazo humlazimisha mtu kutoka kwenye nchi moja hadi nchi nyingine kwa kutafuta kipato Baada ya kupata taarifa kutoka kwa mwalimu huyu, tulitaka kujua namna ambavyo wakurugenzi wa masomo huelewa dhana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka. Kwa upande wa wakurugenzi wa masomo, yafuatayo ni maoni ya mtoataarifa wa pili:

Biashara za kimataifa za kuvuka mpaka ni biashara zinazomruhusu mtu kufanya biashara katika soko linalokusanya wafanyabiashara wa mataifa mengi pamoja katika soko la kimataifa. Pengine, biashara hizi zinaweza kuwa biashara zinazofanyika kutoka nchi moja hadi nyingine.

Chanzo: Data za Uwandani (2023)

Maelezo yaliyotolewa na watoataarifa walioshiriki katika utafiti wetu yanaonesha kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka ni zile zinazofanyika kwenye soko la kimataifa. Vilevile, biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zimefasiliwa kama biashara zinazofanywa na wafanyabiashara kutoka nchi moja kwenda nyingine ili kubadilishana bidhaa au huduma nyingine na wenzao kutoka nchi tofauti. Matokeo ya utafiti huu yanalingana na maelezo ya Vesna, Nikolche na Katerina (2017:105) ambao wanafafanua kuwa biashara ya kimataifa inahusisha shughuli zote za kibiashara zinazofanyika ili kukuza uhamishaji wa bidhaa, huduma, rasilimali, watu, mawazo, na teknolojia katika mipaka ya kitaifa. Biashara ya kimataifa ni kubadilishana mitaji, bidhaa, na huduma katika mipaka au maeneo ya kimataifa.

Maelezo yao yanaonesha kuwa biashara ya kuvuka mipaka ni biashara ya kubadilishana bidhaa, rasilimali, huduma tofauti na mambo mengine kati ya nchi tofauti. Baada la kueleza dhana ya biashara ya kuvuka mipaka, kipengele kinachofuata kinaonesha matokeo ya utafiti kuhusu dhana ya uzungumzaji wa Kiswahili.

3.2 Dhana ya Uzungumzaji wa Kiswahili

Ili kutimiza lengo kuu la utafiti huu la kubainisha nafasi ya biashara ya kuvuka mpaka katika ukuzaji wa uzungumzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Rwanda, tuliona kuwa ni lazima kukusanya taarifa kuhusu dhana ya uzungumzaji wa Kiswahili. Hili lilifanywa ili kuonesha namna ambavyo Kiswahili kinaweza kuendelezwa kupitia biashara za kimataifa za kuvuka mpaka. Taarifa hizo zilipatikana kwa kujibu swali, “Maneno “uzungumzaji wa Kiswahili” yana maana gani kwako kama mwalimu wa Kiswahili? Mtoataarifa wa tatu alijibu yafuatayo:

Kama inavyojulikana, uzungumzaji wa Kiswahili ni uwezo alionao mtu fulani ambao unamwezesha kutumia Kiswahili kwa ufasaha katika mawasiliano.

Chanzo: Data za Uwandani (2023)

Dondoo hili linaonesha kuwa uzungumzaji wa Kiswahili ni umilisi wa kutumia Kiswahili kati ya watu ambapo mmoja humtegea sikio mwenzake akizungumza Kiswahili. Mtoataarifa wa nne, alisema:

Uzungumzaji wa Kiswahi ni utumiaji wa Kiswahili baina ya mtu na mtu, watu na watu, jamii na jamii au kati ya nchi na nyingine kwa maongezi ya ana kwa ana kwa kutumia mdomo au vifaa vya kiteknolojia vinavyoweza kusafirisha sauti ya mtu mmoja hadi kwa mwingine.

Chanzo: Data za Uwandani (2023)

Dondoo hili linaonesha kuwa uzungumzaji wa Kiswahili ni hali ya kutumia Kiswahili kati ya watu wanaozungumza kwa mdomo au kwa vifaa vingine vyenye uwezo wa kusafirisha sauti kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji. Maelezo haya yanathibitishwa na Thornbury (2005) asemaye kwamba lugha ya mazungumzo inahusisha watu wawili au zaidi wanaozungumza kwa kutumia mdomo au sauti bila maandishi. Sehemu ya hapo juu imedhihirisha matokeo ya utafiti kuhusu dhana ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka na uzungumzaji wa Kiswahili. Sehemu inayofuata ni matokeo ya utafiti kuhusu mchango wa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda.

3.3 Mchango wa Biashara za Kimataifa za Kuvuka Mpaka katika Uimarishaji wa Uzungumzaji wa Kiswahili

Lengo la pili la makala hii lilikuwa ni kubainisha mchango wa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Ili kutimiza lengo hili tulijiegemeza kwenye data zilizokusanywa kupitia mahojiano na uchambuzi wa matini. Aidha, ili kutimiza lengo husika, tulijiegemeza katika mhimili wa Nadharia ya Utamaduni Jamii. Mhimili wenyewe ni ule unaoeleza kuwa ujifunzaji wa binadamu ni mchakato wa kijamii. Hii ni kwa kuwa uvumbuzi na ugunduzi huundwa akilini mwa binadamu kutokana na mwingiliano wake na wale walio karibu naye ambao wana ujuzi zaidi yake. Yafuatayo ni matokeo ya utafiti kuhusu lengo la pili katika makala hii.

3.3.1 Kuongeza Motisha ya Kuzungumza Kiswahili kwa Wanafunzi

Matokeo ya utafiti yanadhihirisha kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinawapa motisha wanafunzi na kuwafanya wafurahie kuzungumza Kiswahili. Hii

ni kwa sababu kupitia biashara za kimataifa za kuvuka mpaka wanafunzi wanapata watu wanaozungumza Kiswahili katika familia zao, sokoni, njiani au mahali wanapoishi. Watu hawa huwasaidia wanafunzi kuongeza shauku ya kutaka kujifunza Kiswahili ili nao waweze kukizungumza kwa ufasaha. Hoja hii inathibitishwa na majibu yaliyotolewa na watoataarifa kwa kujibu swali “Je, biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zina mchango gani katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule yenu?” Mtoataarifa wa tano alisema:

Biashara za kimataifa za kuvuka mpaka huwawezesha wanafunzi kukutana na wazungumzaji wa Kiswahili ambao hukuza motisha kwa wanafunzi kwa kuwa huwasababishia kukuza hamu yao ya kutaka kujifunza Kiswahili ili waweze kuzungumza na watu wengine hasahasa wafanyabiashara ambao wanajua Kiswahili tu.

Chanzo: Data za Uwandani (2023)

Dondoo hili linaonesha kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka huwapa motisha wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda na kuwawezesha kuzungumza Kiswahili vizuri. Hii ina maana kwamba biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinawachochea wanafunzi kukuza shauku ya kujifunza Kiswahili ili waweze kuwasiliana na watumiaji wengine wa lugha hii. Tunakubaliana na dondoo hili kwa kuwa motisha ni nyenzo muhimu katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya pili. Matokeo ya utafiti huu yanalingana na matokeo ya utafiti wa Nasser na Majid (2011:995) wanavyoeleza kwamba motisha ina mchango mkubwa katika mchakato wa kujifunza lugha. Walimu wa lugha hawawezi kufundisha stadi za lugha kwa ufanisi ikiwa hawaelewi uhusiano kati ya motisha na athari zake kwa ujifunzaji na upataji wa lugha. Msingi wa motisha ni kile kinachoweza kuitwa shauku, ambayo inahusiana na malengo ya ndani ya mtu na tamaa inayomsukuma kujifunza lugha.

Maelezo ya wataalam hawa hapa juu yanaonesha kuwa motisha ni lazima katika ufundishaji wa lugha. Hivyo basi, tunakubaliana na dondoo hili kwa kuwa kupitia biashara za kimataifa za kuvuka mpaka, wanafunzi wanabahatika kuwasiliana na wazungumzaji wa Kiswahili na kuelewa umuhimu wa Kiswahili katika maisha yao. Mambo haya hukuza hamu ya kujifunza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari zilizopo karibu na mpaka wa Rwanda.

3.3.2 Wanafunzi Kupata Mahali pa Kuzungumza Kiswahili

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinachangia katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Kirehe na Rwamagana. Hii ni kwa sababu biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinawawezesha wanafunzi kupata mahali pa kufanya mazoezi ya kuzungumza Kiswahili. Pia, hukutana na watu wa

kuzungumza nao Kiswahili kwenye shughuli mbalimbali. Jambo hili huwaongezea wanafunzi uwezo wao wa kuzungumza Kiswahili. Mchango huu huthibitishwa na majibu yaliyotolewa na watoataarifa walioshiriki katika utafiti huu. Walionesha kuwa mtu anavyotumia lugha fulani katika shughuli zake za kila siku, ndivyo anavyozidi kuimudu. Kwa mfano, kuna mtoataarifa wa sita aliyesema:

Kama tunavyojua, mtu anavyotumia lugha katika maisha ya kila siku, ndivyo anazidi kuimudu lugha hiyo. Hii ina maana kwamba, mtu anapoishi mahali ambapo lugha fulani hutumiwa, anaimudu lugha hiyo na kuweza kuizungumza kwa muda mfupi. Kwa hiyo, biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinawasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa kuzungumza Kiswahili kwa kuwaweka kwenye mazingira (soko) ambapo Kiswahili hutumiwa mara nyingi na kuwawezesha kukizungumza kwa ufasaha.

Chanzo: Data za Uwandani (2023)

Mtoataarifa ameonesha kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka huwapa wanafunzi wasaa wa kupata mahali pa kuzungumzia Kiswahili kwa muda mrefu. Fursa hii huwaongezea uwezo wa kuzungumza Kiswahili. Maelezo haya yanaungwa mkono na hoja ya mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Utamaduni Jamii inayoeleza kuwa binadamu anaendeleza ujuzi, maadili na imani zake kupitia mwingiliano wake na wanajamii na mazingira anamoishi. Hivyo basi, matokeo ya haya yamethibitisha kwamba biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinakuza Kiswahili cha mazungumzo kwa wanafunzi wa shule sekondari nchini Rwanda kwa kuwajengea mazingira ambapo wanaweza kuzungumza Kiswahili kwa muda mrefu.

3.3.3 Kusaidia Wanafunzi Kuwasiliana na Wazawa wa Kiswahili

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zina mchango usio kifani katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili. Hii ni kwa kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinawasaidia wanafunzi kuwasiliana na wazawa wa lugha ya Kiswahili sokoni, nyumbani au kwenye mazingira wanamoishi. Kwa kuwa kuna wazawa wa Kiswahili ambao hutumia lugha hii kwa ufasaha, biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinawasaidia wanafunzi Wanyarwanda kukuza uwezo wao wa kuzungumza Kiswahili kwa kuwaiga wale wazawa wa Kiswahili wanaotumia lugha hii kwa ufasaha. Wanafunzi wanapowasiliana ana kwa ana na wazawa wa Kiswahili, wanazidi kuimarisha stadi za kuzungumza lugha ya Kiswahili. Wanaiga mifano waliyoipata kutoka kwa wafanyabiashara kutoka kwenye nchi zinazozungumza Kiswahili. Mawazo hayo yanaakisiwa na maelezo yafuatayo ya mtoataarifa:

Wafanyabiashara wa kimataifa ambao ni wazawa wa Kiswahili wanapokuwa wanafanya biashara nchini Rwanda huwa wanatumia lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wanapongea Kiswahili na wazawa wa

Kiswahili, wananufaika kwa kuiga namna bora ya kuzungumza
 Kiswahili na kuanza kujifunza kwa bidii ili nao waweze kuzungumza
 Kiswahili kwa ufasaha

Chanzo: Data za Uwandani (2023)

Matokeo ya utafiti huu hayatofautiani na matokeo ya utafiti uliofanywa na Dörnyei (2009) ambaye anasema kwamba ili mtu ajifunze lugha ya pili ni lazima ajifunze kwa kuiga mfano wa wazawa wa lugha, ambao wana uwezo wa kuzungumza lugha hiyo kwa ufasaha. Kutokana na hayo, kwa kujiegemeza kwenye taarifa tulizozikusanya na kuzichambua, tunakiri kwamba biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zinakuza Kiswahili cha mazungumzo. Biashara kama hizi huwawezesha wanafunzi wa shule za sekondari za mpakani na zilizo mbali na mpaka wa Rwanda kupata na kuongea na wazawa wa Kiswahili. Wazawa hawa wa lugha wanachukuliwa kama mifano ya kuiga ili kuimarisha stadi za kuzungumza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi.

Hali hii inaendana na maelezo ya Palmer (2009) anayesema kwamba wajifunzaji wa lugha ya pili ambao hawana bahati ya kukutana na kuzungumza na wazawa wa lugha, hawawezi kumudu stadi za lugha hasa stadi ya kuzungumza lugha kwa muda mfupi. Vilevile, wazo hili huakisi mhimili wa Nadharia ya Utamaduni Jamii usemao kwamba ujifunzaji wa lugha ni mchakato wa kijamii, uvumbuzi na ugunduzi huundwa akilini mwa binadamu kutokana na mwingiliano wake na wale walio karibu naye ambao wana ujuzi zaidi.

3.3.4 Kuondoa Imani Potofu kuhusu Kiswahili

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha pia kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka huimarisha uzungumzaji wa Kiswahili kwa kuwa hushiriki katika kuondoa imani potofu miongoni mwa wanafunzi. Baadhi ya wanafunzi huichukulia lugha ya Kiswahili kama lugha isiyo na umuhimu. Hivyo, biashara za kimataifa za kuvuka mpaka huwaonesha wanafunzi umuhimu wa Kiswahili kwenye soko la ajira. Kama wanafunzi wataondoa imani potofu waliyonayo kuhusu Kiswahili, watajifunza kwa bidii lugha hii ili waweze kuimudu vyema katika mazungumzo. Yafuatayo ni maoni ya mtoataarifa mwingine kuhusu mchango wa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka katika kukuza Kiswahili cha mazungumzo:

Ndiyo, biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zina mchango mkubwa katika kukuza Kiswahili cha mazungumzo kwa wanafunzi wetu. Ushahidi ninaoweza kutoa ni mwanafunzi mmoja katika shule yetu aliyetuambia kwamba alichagua kusomea mchepuo wa lugha kutokana na utamu aliouhisi wakati alipowaona madereva wa malori makubwa yanayobeba bidhaa kutoka Tanzania. Mwanafunzi huyu alisema kwamba madereva hawa walikuwa wanatumia lugha ya Kiswahili kwa kuwa hawakujua lugha ya Kinyarwanda. Katika mazingira haya, walihitaji mtu anayeweza kuwaelekeza njia lakini hawakumpata kutokana na kuwa watu wote waliokuwa hapo karibu na barabara ya

Rwamagana - Kigali hawakujua Kiswahili. Yeye alipata uamuzi wa kusomea mchepuo wa lugha (LKK) ili aweze kuvuna manufaa yatokanayo na kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha.

Chanzo: Data za Uwandani (2023)

Dondoo hili linathibitisha umuhimu wa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka kwa kuonesha kuwa biashara hizi zinaondoa imani potofu kuhusu Kiswahili na hivyo kuwapa motisha wanafunzi kujifunza Kiswahili kwa bidii. Kwa hiyo, mtu anayeona kuwa lugha inaweza kumfaa katika maisha yake, atajitahidi kuisoma ili aweze kuizungumza kwa ufasaha. Maelezo haya yanalingana na matokeo ya utafiti wa Smith (1971) asemaye kwamba kama mwanafunzi ana imani potofu kuhusu lugha ya pili, itakuwa vigumu kwake kuweza kuzungumza lugha hiyo. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka huimarisha uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda kupitia wafanyabiashara wanaotumia Kiswahili katika shughuli zao.

4.0 Hitimisho

Utafiti huu ulihusu kubainisha nafasi ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili katika shule za mpakani na zilizo mbali na mpaka wa Rwanda. Makala hii imeonesha kuwa ingawa jitihada nyingi zimefanyika ili kuimarisha lugha ya Kiswahili, bado idadi ya Wanyarwanda wanaoweza kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha ni ndogo kama ilivyothibitishwa na Tabaro (2019). Licha ya hayo, matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa biashara za kimataifa za kuvuka mpaka zina mchango mkubwa katika uimarishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Hii ni kwa kuwa biashara za kuvuka mpaka zinaleta manufaa yafuatayo: mosi, kuongeza motisha ya kujifunza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Pili, kuwapa wanafunzi mahali pa kuzungumza Kiswahili. Tatu, kutoa fursa kwa wanafunzi kuwasiliana na wazawa wa lugha ya Kiswahili na nne ni kuondoa imani potofu kuhusu Kiswahili. Aidha, makala inatoa wito kwa wanafunzi wa Kiswahili pamoja na walimu wao kutumia ipasavyo fursa ya biashara za kimataifa za kuvuka mpaka ili kukuza uwezo wa kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha.

Marejeleo

- Chiragdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Dörnyei, Z. (2009). "Motivation, Language Identity and the L2 Self. *Multilingual Matters*." 36(3): 9-42.

- Guevara, B. na Teresa, M. (2019). *Trans Border Testimonies of Language Learning and Socialization*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha New Mexico.
- Morosini, P. na Singh, H. (1994). "Post-cross-border Acquisitions: Implementing 'National Culture-compatible' Strategies to Improve Performance." *European Management Journal*. 12(4): 390-400. Inapatikana katika [https://doi.org/10.1016/0263-2373\(94\)90025-6](https://doi.org/10.1016/0263-2373(94)90025-6). Ilisomwa tarehe 20/6/2023.
- Mwakagele, C. (2016). *Lugha ya Kiswahili Ipewe Nafasi Inayostahili: Muungwana Lazima Nilonge*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Nasser, O. na Majid, V. (2011). "Motivation, Attitude and Language Learning." *Procedia - Social and Behavioral Sciences*. 2(29): 994-1000.
- Otieno, E.A. (2020). Ufundishaji wa Sarufi ya Kiswahili kwa Watoto wenye Matatizo ya Kusikia katika Shule za Msingi Nchini Kenya. (Tasnifu ya Umahiri). Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Masinde Muliro.
- Palmer, K.A. (2009). "Understanding Human Language: An In-depth Exploration of the Human Facility for Language." *Inquiries Journal*. 1(12): 1-12.
- Smith, A.N. (1971). "The Importance of Attitude in Foreign Language Learning." *Modern Language Journal*. 55(2): 83-88.
- Tabaro, J.C. (2019). *Slow Pick up of Kiswahili, Rwanda's Latest Official Language*. Kigali: KT Press.
- Thornbury, S. (2005). *How to Teach Speaking*. Harlow, England: Longman.
- Vesna, G., Nikolche, J. na Katerina, B. (2017). "International Business and Trade." *International Journal of Sciences: Basic and Applied Research (IJSBAR)*. 31(3): 105-114.
- Vygotsky, L.S. (1962). *Thought and Language*. London: MIT Press.
- Zubaidi, N. (2015). *Sociocultural Theory Scholarship View Project Teacher's Cognition in the Provision of Corrective Feedback: Case Study on Indonesian EFL Teachers View Project*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Malang.